


HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO

Simu/Fax Na: 023 – 2614727
Simu ya Upepo "Mji"
e-mail-mmctownhall@morogoro.net



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa
S.L.P. 166
MOROGORO - TANZANIA

**TANGAZO LA ZABUNI ZA UWAKALA WA KUJENGA , KUENDESHA NA
KUKABIDHI MRADI WA UJENZI WA CHOO CHA UMMA ENEO LA MASIKA
ZABUNI NA. LGA/079/2018-2019/HQ/W/11**

Tarehe: 08/01/2019

WW

1. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inakusudia kutafuta mbia atakayejenga, kuendesha na kurejesha mradai wa ujenzi wa choo cha Umma eneo la Masika Manispaa ya Morogoro.
2. Halmashauri inakaribisha maombi ya zabuni ya ubia wa kujenga, kuendesha na baadaye kurejesha kwa mwenye mali kitega uchumi cha Choo kilichoko maeneo ya nanenane Manispaa ya Morogoro. Mzabuni atatakiwa kujenga kwa kutumia mchoro na BOQ iliyoambatanishwa kwenye nyaraka ya zabuni. Wazabuni mbalimbali wenye sifa, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hii kwa niaba ya Halmashauri wanaombwawaombe zabuni hii.
3. Wazabuni wenye nia ya kufanya kazi hii wana weza kukagua Nyaraka za zabuni kwenye ofisi ya Ugavi kuanzia saa 1:30 hadi saa 9:30 Alasiri siku za kazi Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu za Kitaifa.

MASHARTI YA JUMLA NA MAALUM KWA WAOMBAJI WOTE:

1. Mwombaji aambatanishe leseni ya biashara husika.
2. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.
3. Mwombaji atoe uthibitisho wa uwezo wa kifedha (financial capacity) alionao ili kuthibitisha uwezo wa kutekeleza zabuni.
4. Mwombaji aambatanishe orodha ya watumishi alionao na vitendea kazi.
5. Mwombaji aambatanishe mchanganuo unaoonyesha gharama atakazotumia kujenga, mapato atakayokusanya kwa mwaka anategemea kurejesha gharama zake za Ujenzi kwa muda gani, matumizi yake na kiasi gani atatoa kwa Halmashauri kwa mwezi.

6. Mkataba utakao tolewa utategemea urejeshaji wa gharama na faida itakayopatikana.
7. Mwombaji atakayepitishwa na bodi ya zabuni ya Halmaashauri ya Manispaa atalazimika kuweka dhamana ya pesa taslimu yenye thamani sawa na kiasi alichoomba kuilipa Halmashauri kwa mwezi baada ya ujennzi kumalizika na uendeshaji kuanza na itarudishwa baada ya Mkataba kumalizika.
8. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuilipa Halmashauri kodi ya kila mwezi ambayo italipwa mapema (in-advance) kabla ya mwezi husika kuanza kwa kipindi chote cha Mkataba.
9. Mwombaji atakayeshinda zabuni atalazimika kukusanya viwango halali vilivyoidhinishwa na sheria mama na sheria ndogondogo za Halmashauri.
10. Waombaji wenye makampuni waambatanishe nyaraka zote muhimu za kampuni.
11. Mzabuni atatumia mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.
12. Mzabuni atatakiwa kutaja wakurugenzi/mkurugenzi wa kampuni na mahali ofisi ya kampuni ilipo na aambatanishe “company profile”
13. Nyaraka za Zabuni zinapatikana kwa kuleta barua ya maombi na malipo ya fedha taslimu yasiyorudishwa (Non refundable) ya shilingi elfu hamsini tu (Tshs **100,000/=**) kwa Mkurugenzi wa Manispaa S.L.P 166 Morogoro.
14. Zabuni zote ziwasilishwe kwenye sanduku la zabuni lililopo katika ukumbi wa mikutano wa Manispaa ya Morogoro au zitumwe kwa kifurushi maalum (registered mail) ili zifike kabla ta tarehe na muda wa mwisho wa uwasilishaji zabuni na zitumwe kwa:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
S.L.P 166
Morogoro**

15. Mwisho wa kuzipokea zabuni ni siku ya Jumanne tarehe 22/01/2019 saa 6.00 Mchana na mara baada ya hapo Zabuni zitafunguliwa kwenye ukumbi wa mikutano wa Manispaa, waombaji au wawakilishi wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi. Bahasha ya nje iandikwe Zabuni Namba na Jina la Zabuni na ISIFUNGULIWE KABLA YA SAA 6:00 MCHANA Tarehe 22/01/2019.
16. Zabuni zilizochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielektroniki na ambazo hazikupokelewa, na hazikufunguliwa na hazikusomwa mbele ya hadhara kwenye sherehe ya ufunguzi hazitakubaliwa kufanyiwa tathmini.

John k.Mgalula
Mkurugenzi wa Manispaa
Morogoro.